JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA

Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2340012 | Fax:+255(0)26 2340014

Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA


# TAARIFA FUPI YA WAKALA KWA WAZIRI WA KILIMO MHESHIMIWA DKT. CHARLES JOHN TIZEBA

## 1.0 UTANGULIZI

Dhana ya usalama wa chakula nchini imekuwepo tangu enzi za ukoloni ambapo kufuatia majanga mbalimbali kama vile ukame, mafuriko, nk. Serikali iliwajibika kuchukua hatua madhubuti za kuwasaidia wananchi wake ili wasife kwa njaa. Dhana ya usalama wa chakula nchini ilipewa umuhimu wa kipekee baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 ambapo serikali ilitilia mkazo kilimo cha mazao ya chakula ili kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ambayo wananchi walihimizwa kuitunza na kuihifadhi vizuri kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997. Hati ya kuanzisha rasmi Wakala ilitolewa mwaka 2008 [The Executive Agency (The National Food Reserve Agency) (Establishment) Order, 2008] na Wakala kuanza majukumu yake Julai 2008.

Wakala ulinzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini ili kukabiliana na upungufu wa chakula kwa njia ya kununua, kuhifadhi na kutoa chakula pale kinapohitajika kwa dharura kwa kuzingatia ufanisi na tija.

### 1.1 Dira:

Kuwa taasisi yenye uwezo wa kukabiliana na upungufu wa chakula kwa wakati ifikapo mwaka 2020.

### 1.2 Dhamira:

Kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula kwa ufanisi na tija.


### 1.3 Majukumu mahususi ya NFRA ni kama ifuatavyo:

(i) Kununua na kuhifadhi akiba ya chakula;
(ii) Kuzungusha (re-cycling) akiba ya chakula;
(iii) Kutoa chakula kwa waathirika waliokumbwa na upungufu wa chakula kwa maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa.

## 2.0 MUUNDO WA WAKALA

Wakala unaongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu ambaye huteuliwa na Waziri mwenye dhamana kwa kushauriana na Katibu Mkuu. Afisa Mtendaji Mkuu anasaidiwa na Wakurugenzi watatu ambao ni Mkurugenzi wa Uendeshaji, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu, Mameneja wa Kanda na Wakuu wa Vitengo vinne vya Ukaguzi wa Ndani, Ununuzi, Sheria na Udhibiti Fedha.

Mkurugenzi wa Uendeshaji anasaidiwa na Meneja wa Uendeshaji na Meneja wa Uthibiti Ubora na Uhifadhi; Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara anasaidiwa na Meneja wa Mipango na Uwekezaji, Meneja wa Masoko na Meneja wa Tehama, na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu anasaidiwa na Meneja wa Rasilimaliwatu na Utawala na Meneja wa Majengo Miliki na Mazingira. Wakala hutekeleza majukumu yake kupitia kanda zake saba (Makambako, Songea, Sumbawanga, Kipawa, Dodoma Arusha na Shinyanga) ambazo zimewekwa kimkakati.




*Mchoro Na.1: Muundo wa Wakala*

## 3.0 UWEZO WA HIFADHI

NFRA ina maghala 34 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 251,000 kwa sasa. Mgawanyo wa mikoa kikanda pamoja na uwezo wa uhifadhi kikanda umeainishwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na.1: Uwezo wa hifadhi ya Chakula**

| Kanda | Uwezo wa Hifadhi | Mikoa |
|---|---|---|
| Arusha | 39,000 | Arusha, Kilimanjaro na Manyara |
| Kipawa | 52,000 | Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Mtwara na Lindi |
| Dodoma | 39,000 | Dodoma na Singida |
| Shinyanga | 14,500 | Shinyanga, Tabora, Mwanza, Mara, Kagera, Geita, Simiyu na Kigoma |
| Makambako | 39,000 | Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe |
| Songea | 29,000 | Ruvuma |
| Sumbawanga | 38,500 | Rukwa na Katavi |
| **Jumla** | **251,000** | |



*Picha Na. 1: Magunia ya mahindi yaliyohifadhiwa vizuri katika ghala*



*Picha Na.2: Ghala la kuhifadhia Nafaka*

# 4.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WAKALA

## 4.1 Kununua Akiba ya Chakula

Mazao yanayonunuliwa kwa sasa ni mazao ya nafaka hususan mahindi. Mazao haya hununuliwa kupitia Kanda za Wakala katika maeneo yaliyobainika kuwa na uzalishaji wa ziada wa chakula, hususan vijijini. Aidha, katika zoezi hili maandalizi hufanywa kwa kushirikiana na Mikoa pamoja na Halmashauri zitakazo, husika katika ununuzi. Elimu kuhusu ubora wa nafaka na vigezo hutolewa kwa wakulima na watumishi wanaohusika na ununuzi. Zoezi la ununuzi huanza mwezi Julai na kumalizika Desemba kila mwaka.

Wakala hutumia njia zifuatazo katika ununuzi wa chakula kwa ajili ya akiba ya Serikali.

i. **<u>Vituo vya Ununuzi</u>**: Wakala hutumia vituo vya ununuzi ikiwa ni pamoja na vile ambavyo vinahamishika (mobile collection center).
ii. **<u>Vikundi/SACCOS/AMCOS</u>**: Wakala hubaini vikundi na Taasisi za Wakulima kama vile AMCOS, SACCOS ambazo ziko tayari kuuza nafaka kwa Wakala na kuingia nazo mikataba kwa lengo la kuimarisha ushirika nchini.
iii. **Kutumia Mawakala:** Wakala hubaini na kuingia mikataba na mawakala wa kuuza mahindi kwa Wakala lengo likiwa ni kusogeza huduma kwa wakulima katika maeneo ambayo NFRA haina vituo vya ununuzi.
iv. **Kutumia Zabuni:** Kutangaza zabuni za wazi hususan katika maeneo yenye uzalishaji mdogo ili wazabuni watakaoshinda wapeleke mahindi katika maghala ya Wakala yaliyoko maeneo hayo.
v. Ifuatayo ni orodha ya vigezo vinavyozingatiwa wakati wa ukaguzi wa ubora wa mahindi.

**Jedwali Na.2: Vigezo vya Ubora wa Mahindi**

| Na. | Vigezo | Kiwango cha juu (%) |
|---|---|---|
| 1. | Kukauka/Unyevunyevu | 13% |
| 2. | Takataka | 0.5% |
| 3. | Punje zilizovunjika | 2% |
| 4. | Punje zilizoliwa na wadudu | 1% |
| 5. | Punje zilizosinyaa/zilizooza | 1% |
| 6. | Punje mbovu/zilizooza | 2% |
| 7. | Punje za rangi tofauti | 0.5% |
| 8. | Punje zisiwe na sumu, aina yoyote ile ya uvundo au viuatilifu visinyotakiwa. | Hakuna |

## 4.2 Akiba ya Chakula

### Jedwali Na.3: Mchanganuo wa Akiba ya Chakula

| WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA (NFRA)<br>Akiba ya Chakula Hadi Tarehe 12/03/2018 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kanda | Kituo | Akiba kuanzia Tarehe 1/7/2017 | Ununuzi wa msimu 2017/18 hadi tarehe 12/03/2018 | | Jumla Salio+Ununuzi | Matoleo | Uhamishaji (Kutoka) | Uhamishaji (Mapokezi) | Akiba Ghalani |
| | | Mahindi | Lengo | Utekelezaji | | | | | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| Arusha | Arusha | 3,543.618 | 1,000.000 | 1,000.000 | 4,543.618 | 3,007.280 | - | 2,446.259 | 3,982.597 |
| Dodoma | Dodoma | 3,088.538 | 1,500.000 | 1,100.000 | 4,188.538 | 905.659 | 339.629 | 3,017.551 | 5,960.801 |
| | Manyoni | 3,081.788 | - | 400.000 | 3,481.788 | - | - | - | 3,481.788 |
| Kipawa | Kipawa | 8,574.917 | - | - | 8,574.917 | 204.768 | 2,024.817 | 1,290.142 | 7,635.474 |
| Makambako | Makambako | 11,330.974 | 8,700.000 | 3,474.203 | 14,805.177 | 139.890 | - | - | 14,665.287 |
| | Mbozi | 1,013.552 | - | 5,487.317 | 6,500.869 | 1,013.552 | - | - | 5,487.317 |
| Shinyanga | Shinyanga | 4,726.942 | - | - | 4,726.942 | 641.961 | - | 40.597 | 4,125.578 |
| | Kasulu | 111.629 | - | - | 111.629 | 111.629 | - | - | 0.000 |
| | Bukene | 1,829.994 | - | - | 1,829.994 | 395.000 | - | 2,024.480 | 3,459.474 |
| Songea | Songea | 10,335.395 | 11,482.000 | 11,557.529 | 21,892.924 | - | - | - | 21,892.924 |
| Sumbawanga | Sumbawanga | 13,989.278 | - | - | 13,989.278 | - | 1,938.462 | - | 12,050.816 |
| | Laela | 4.606 | 3,000.000 | 3,019.594 | 3,024.200 | - | - | 1,649.350 | 4,673.550 |
| | Mpanda | 7,261.970 | - | - | 7,261.970 | 134.000 | 4,972.162 | 288.919 | 2,444.727 |
| | ON-TRANSIT | 1,501.317 | - | - | 1,501.317 | - | - | - | 2.937 |
| **Jumla** | | **70,394.518** | **25,682.000** | **26,038.643** | **96,433.161** | **6,553.739** | **9,275.070** | **10,757.298** | **89,863.270** |
| | **Jumla Akiba ya Kuanzia** | **70,394.518** | | | **Jumla Mauzo** | **6,553.739** | **Akiba Ghalani** | | **89,863.270** |

## 4.3 Kuzungusha Akiba ya Chakula

Wakala hudhamiria kuhifadhi nafaka kwenye maghala kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu. Ili kuongeza usambazaji wa nafaka katika masoko, Wakala huingiza chakula katika masoko yaliyobainika kuwa na upungufu wa chakula. Aidha, Wakala huuza chakula kwa taasisi mbalimbali ili kukidhi mahitaji kwa wakati. Uuzaji wa nafaka husaidia Wakala kupata nafasi kwa ajili ya ununuzi wa mazao mapya na fedha za kununua mazao mpya.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala umepanga kuzungusha mahindi ambayo yamekaa ghalani zaidi ya miaka mitatu, ambapo tayari Wakala umepata kibali kutoka Wizara ya Kilimo kuuza jumla ya tani 25,000 za mahindi. Mauzo haya ni fursa kwa Wakala kuuza akiba iliyokaa ghalani muda mrefu hivyo kuweza kuepuka kuharibika kwa akiba ya chakula, kupata nafasi ya kuhifadhi mazao mapya msimu ujao na kuhakikisha ubora wa akiba ya chakula kilichohifadhiwa katika maghala ya Wakala wakati wote.

Hadi kufikia leo Wakala umeweza kuuza jumla ya tani 1,800 za mahindi kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA). Mahindi haya yameuzwa kwa Shilingi 720/kg. Mauzo haya yamewezesha Wakala kupata pesa kiasi cha Shilingi Bilion1.2.

Aidha, Wakala unaendelea kutekeleza mkataba wa kuuza tani 20,000 za mahindi kwa Mpango wa Chakula Duniani (WFP) baada ya kushinda zabuni. Katika Mkataba huu Wakala unauza mahindi kwa U$ 264/tani. Tayari Wakala umeuza tani 4,753.739 Kwa WFP kupitia Mkataba huu. Baada ya kukamilika mauzo haya Wakala utapata pesa takribani Shilingi Bilion 11.

Pamoja na kuwezesha Wakala kupata pesa za kuanzia ununuzi msimu ujao, mauzo haya yameupatia Wakala fursa ya kuhamisha mahindi yaliyokuwa yamehifadhiwa katika maghala ya Kanda ya Sumbawanga ambapo maghala mengine yalikuwa yamekodishwa na yalikuwa chakavu sana. Kuuzwa kwa mahindi ya kanda ya Sumbawanga pia kumewezesha upatikanaji wa nafasi kwa ajili ya kutunza nafaka itakayonunuliwa msimu ujao. Pia kutawezesha kufanyika kwa shughuli ya mradi zinazoendelea.

**Jedwali Na.4: Mpango wa Kuzungusha Akiba ya Chakula**

| MUHTASARI WA AKIBA YA CHAKULA KWA MISIMU YA UNUNUZI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| AKIBA YA CHAKULA HADI 12/03/2018 | | | | | | |
| KANDA | 2013/2014 | 2014/2015 | 2015/2016 | 2016/2017 | 2017/2018 | JUMLA |
| ARUSHA | | | | 2,982.597 | 1,000.000 | 3,982.597 |
| DODOMA | | | | 7,942.589 | 1,500.000 | 9,442.589 |
| KIPAWA | | | 1,636.196 | 5,999.278 | | 7,635.474 |
| MAKAMBAKO | | | 453.556 | 10,737.528 | 8,961.520 | 20,152.604 |
| SHINYANGA | | | 4,366.005 | 3,219.047 | | 7,585.052 |
| SONGEA | | | | 10,335.395 | 11,557.529 | 21,892.924 |
| SUMBAWANGA | | | | 16,149.499 | 3,019.594 | 19,169.093 |
| On-Transit | | | | | | 2.937 |
| JUMLA KUU | - | - | 6,455.757 | 57,365.933 | 26,038.643 | 89,863.270 |

## 5.0 MAFANIKIO

Wakala umefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kila mwaka, baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na: -

i. Kuwa soko la mahindi kwa wakulima hivyo kuweza kununua sehemu ya ziada ya zao la mahindi kutoka kwa wakulima na kutimiza malengo yaliyowekwa na Serikali kila mwaka.

ii. Kutoa Chakula cha msaada kwa waathirika: Kila inapolazimika, NFRA imekuwa ikisimamia kwa ufanisi utoaji wa chakula cha njaa kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

iii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Endelevu-2030 (*Sustainable Develelopment Goals*): Wakala unaendelea kutekeleza mikakati ya kuhakikisha usalama wa chakula (*Zero hunger*) kwa kuhakikisha kuna akiba ya chakula ambacho ni salama kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya dharura nchini.

## 6.0 FURSA ZA WAKALA ILI KUONGEZA UFANISI

i. Kuongeza uwezo wa kuhifadhi ili kuendana na ongezeko la idadi ya watu na kuchangia jitihada za Wizara ya kilimo kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno (*postharvest loss*).
ii. Kutumia Mifumo na Teknolojia ya kisasa kutathimini na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wakala (*tracking systems, data base, security cameras etc*).
iii. Kutumia Teknolojia za kisasa za kuhifadhi (*silo complexes*) na utekelezaji wa Sera ya Serikali ya awamu ya tano ya kufikia uchumi wa kati kwa kujenga Tanzania ya viwanda.
*iv.* Kuongezewa fedha za ununuzi wa nafaka ili kuwa na akiba ya chakula ya kutosha kwa ajili ya dharura wakati wote (*robby for increased government subvention for grain procurement, Funds from international NGO's and strategic recycling).*
*v.* Kuhakikisha ubora na usalama wa akiba ya chakula ya Taifa wakati wote *(effective quality management).*

## 7.0 WAKALA UNAENDELEA KUTEKELEZA MIKAKATI IFUATAYO ILI KUTUMIA FURSA ZILIZOPO

i. Kuimarisha rasilimali watu ya Wakala
ii. Kuongeza uwezo wa uhifadhi kutoka tani 251,000 za sasa hadi kufikia malengo ya tani 501,000 ifikapo 2019/2020. Malengo haya yatafikiwa kupitia utekelezaji wa mradi kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Poland. Aidha, Wakala unaendelea kufanya majadiliano na taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi pamoja na wawekezaji binafsi ili kupata fedha zaidi zitakazowezesha kutekeleza mipango ya maendeleo ya Wakala ikiwa ni pamoja na azma ya Serikali ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka hadi kufikia tani 1,000,000.
iii. Kuboresha mifumo ya utendaji kazi ikiwemo matumizi sahihi na stahiki ya TEHAMA.
iv. Kupanua wigo wa mapato ikiwa ni pamoja na kushirikiana na sekta binafsi katika kuwekeza katika miundombinu na teknolojia za kisasa za kuhifadhi.
v. Kutoa elimu kwa Wakulima juu ya viwango vya ubora wa mahindi

vi. Kujiendesha kibiashara bila kuathiri jukumu la kuhakikisha akiba ya chakula kwa ajili ya dharura.

## 8.0 MRADI WA KUONGEZA UWEZO WA KUHIFADHI

Mradi utagharimu Dola za Kimarekani Milioni 55 millioni, ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Poland. Mradi utatekelezwa na kampuni mbili za Kandarasi kutoka Poland (Feerum na Unia Araj) ambapo msimamizi wa utekelezaji wa mradi ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

Mradi utahusisha ujenzi wa vihenge vya kisasa, maghala ya kisasa pamoja na ukarabati wa ofisi. Mradi utakekelezwa katika maeneo nane ambayo ni Arusha (Babati), Dodoma, Makambako, Mbozi, Shinyanga, Songea, Sumbawanga na Mpanda. Baada ya mradi kukamilika Wakala utakuwa umeongeza uwezo wa kuhifahi kwa 250,000 MT zaidi (vihenge vya kisasa 190,000MT na maghala 60,000 MT).

Kupitia barua ya tarehe 18 Januari 2018, Wizara ya Fedha na Mipango imeujulisha Wakala kuanza rasmi kwa utekelezaji wa mradi tarehe 09 Desemba, 2018. Hivyo utekelezaji wa mkataba kati ya NFRA na Wakandarasi umeanza rasmi tarehe 9 Desemba, 2017.

**Jedwali Na. 5: Maeneo ya Utekelezaji wa Mradi**

| KANDA ZA WAKALA | ENEO LA UJENZI KATIKA KANDA | AINA YA UJENZI | | GHARAMA ZA UJENZI (USD) | MKANDARASI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | VIHENGE | GHALA | | |
| **Arusha** | Babati | 25,000 | 15,000 | **8,080,650.00** | **Unia Araj Realizacje** |
| **Dodoma** | Dodoma | 20,000 | | **4,823,325.86** | **Feerum S.A** |
| **Shinyanga** | Shinyanga | 20,000 | 10,000 | **6,622,898.40** | **Feerum S.A** |
| **Makambako** | Makambako | 20,000 | 20,000 | **6,324,195.94** | **Feerum S.A** |
| | Mbozi | 20,000 | | **5,202,547.65** | **Feerum S.A** |
| **Songea** | Songea | 45,000 | 10,000 | **10,167,823.96** | **Feerum S.A** |
| **Sumbawanga** | Sumbawanga | 20,000 | | **6,019,399.00** | **Unia Araj Realizacje** |
| | Mpanda | 20,000 | 5,000 | **6,180,857.00** | **Unia Araj Realizacje** |
| **Total** | | **190,000** | **60,000** | **53,421,697.81** | |

### 8.1 Malipo ya Awali kwa Wakandarasi (*Advance Payment*)

**Kampuni ya Kandarasi Feerum S.A** imewasilisha ankara yake ya kwanza kwa ajili ya malipo ya awali (advance payment) ya Dola za Kimarekani Milioni 4.9 ambayo ni 15% ya mkataba wake na NFRA wa ujenzi wa vihenge na maghala ya kisasa. NFRA ilipokea Ankara hiyo tarehe 18 Januari 2018 na kupitia Mratibu wa Mradi na Meneja wa Mradi (TBA) ankara hiyo ya malipo ya awali ilihakikiwa na idhini ya malipo hayo imetolewa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa barua ya tarehe 23 Januari 2018 kwa ajili ya malipo kwa kuzingatia utaratibu uliopo katika Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Poland.

**Kampuni ya Kandarasi ya Unia Araj Realizacje Sp. Zo.o**, imewasilisha kwa mara nyingine ankara yao ya kwanza kwa ajili ya malipo ya awali tarehe 27 Febuari 2018 katika Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, ankara hiyo iliyowasilishwa Wizara ya Fedha bado haijawasilishwa NFRA kwa ajili ya kuhakikiwa na kutolewa idhini ya malipo, hivyo Wakala unaendelea na ufuatiliaji na kuhaikikisha ankara hiyo inawasilishwa kwao mapema ili iweze kuendelea na taratibu za malipo.

### 8.2 Mandalizi ya Ujenzi

#### 8.2.1 Usajili

Taratibu za usajili na utambuzi BRELA zimekamilika kwa Kampuni zote mbili za Kandarasi. Aidha Kampuni ya Feerum S.A imepata usajili wa muda wa daraja la kwanza kutoka Bodi ya Usajili wa Kandarasi (CRB), na kwa sasa wapo katika taratibu za kuomba usajili wa wakandarasi wao katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) na kuwaombea vibali vya kazi nchini kupitia Idara ya Uhamiaji. Kwa upande wa Kampuni ya Unia Araj Realizacje Sp Zo.o tayari wamepata usajili wa Wakandarasi wao katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) na kwa sasa wanaendelea na maandalizi usajili katika Bodi ya Usajili wa Kandarasi (CRB) pamoja na kuwaombea vibali vya kazi wahandisi wao wasio watanzania.

#### 8.2.2 Maandilizi ya Vitendea Kazi kwa ajili ya Mradi

Kontena 43 za Kampuni ya Feerm S.A, zenye vifaa vya vihenge tayari zipo bandari ya Dar es Salaam na taratibu za forodha zinaendelea ili kontena hizo ziweze kutolewa, pia kuna kontena zingine 51 zipo njiani kuwasili bandari ya Dar es Salaam. Aidha, mitambo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi vikiwemo, *Excavator*, *Bulldozer* na *Backhoe /Front loader* tayari vimeshawasilishwa

katika maeneo matano (5) ya ujenzi yanayosimamiwa na Kampuni ya Feerum S.A.

### 8.2.3 Vibali vya Ujenzi

Michoro kwa ajili ya kupata vibali vya ujenzi imekamilika kwa maeneo matano ya ujenzi yatakayo jengwa na Kampuni ya Feerum S.A, hivyo taratibu za uombaji wa vibali vya ujenzi katika maeneo hayo utaanza hivi karibuni. Michoro kwa maeneo mengine matatu yatakayo jengwa na Kampuni ya Unia Araj Realizacje Sp zo.o itawasilishwa katikati ya mwezi Machi kwa ajili ya kuidhinishwa na kuombea vibali vya ujenzi.

### 8.2.4 Maboresho ya usanifu wa ghala la Sumbawanga ili liwe na uwezo wa kuhifadhi zaidi ya tani 20,000

Kwa mujibu wa Kampuni ya Unia Araj Realizacje Sp zo.o, sanifu ya kotesheni na michoro kwa ajili ya ghala la Sumbawanga upo katika 90% kukamilika, hivyo katikati ya mwezi Machi kotesheni na michoro husika itakuwa imekamilika na kuwasilishwa kwa Meneja wa Mradi (TBA) kwa ajili ya mapitio.

### 8.2.5 Faida za mradi

Mradi huu ni jitihada za Serikali ambazo zitapelekea ukuwaji wa uchumi nchini na kuchangia kuwezesha Tanzania ya viwanda. Kuongezeka wa uwezo wa kuhifadhi kutawezesha maghala ya Wakala kuweza kuhifadhi akiba ya Chakula ambayo itaendana na mahitaji halisi ya dharura kulinganisha na ongezeko wa watu nchini. Hifadhi ya Chakula inayohitajika kukidhi mahitaji ya dharula kwa miezi mitatu ni zaidi ya tani 500,000 ukilinganisha na tani 150,000 iliyokuwa inahitajika miaka ya 1992 Wakala ulipoanzishwa.

Aidha, technologia ya vihenge itawezesha Wakala kutumia teknolojia ya kisasa na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji; Itawezesha Wakala kuhifadhi chakula kwa muda mrefu Zaidi; itasaidia kupunguza upotevu wa zao la mahindi baada ya kuvuna (*posthaverst loss*) na kuongeza soko la mahindi nchini na kuimalisha usalama wa nafaka inayohifadhiwa kwa kudhibiti sumukuvu (*Aflatoxin*) kwa mahindi yaliyohifadhiwa.

*'Tanzania ya Viwanda, NFRA pia tunatekeleza'*

Kwa heshima, Nawasilisha.

Vumilia L. Zikankuba

**Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu**